JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE

SHULE YA SEKONDARI
KIJOMBE,
S.L.P 64,
MAKAMBAKO.
TAREHE …../ …../ …….
Mob: 0755926536

JINA LA MWANAFUNZI……

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIJOMBE ILIYOPO WILAYA YA WANGING'OMBE MKOA WA NJOMBE MWAKA –2021

Utangulizi:

Ninayo furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Kijombe. Shule ipo kata ya Kijombe umbali wa km 8 kutoka lami Soliwaya, nauli kutoka mjini ni Tsh. 2500/=. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **11/01/2021.** Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **10/01/2021 hadi tarehe 18/01/2021** ndani ya siku saba(7).

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:

I. SARE ZA SHULE

A) KWA UPANDE WA WASICHANA

Ni suruali mbili (02) nyeusi zisizo za mng'ao na gauni mbili (02) nyeupe kora ya mviringo na marinda kutoka kitovoni na kuishia magotini, traki suti(02) blue-bahari au dark blue kwaajili ya michezo, viatu vyeusi pea mbili (02) soksi nyeupe pea mbili (02), hijabu ifanane na rangi ya gauni pamoja na masweta mawili (02) rangi ya zambarau.

B) KWA UPANDE WA WAVULANA ,

Suruali nyeusi mbili (02) zisizo za mng'ao, mashati meupe mawili (02) mikono mirefu na tai nyeusi, viatu vyeusi pea mbili (02), soksi nyeusi pea mbili (02), traki suti za zambarau pea mbili(02, masweta mawili (02) rangi ya zambarau.

C) KWA WOTE:

- Aje na godoro moja, shuka za pinki au blue bahari pea mbili (02), vifaa vya kutunzia maji, vifaa vya kuogea au kufulia, vifaa vya kunywea uji pamoja na vifaa vya kulia chakula. **Vitakaguliwe na mwalimu wa Bweni**

- Daftari 10 counter book Q2, kalamu na mkebe wa hesabu.

- Rimu moja A4 (bunda la karatasi) liletwe Shuleni

- Sare ya kazi ni gauni mbili (02) rangi ya Pinki kwa wasichana na kwa wavulana suruali mbili (02) rangi ya damu ya mzee.

- Nguo za nyumbani hazihitajiki hapa Shuleni.

- Vifaa vya usafi ni **kwanja moja**, **jembe moja lenye mpini imara**, **ufagio**, **kindoo cha lita kumi (10)** au **dishi moja**. **Vitapokelewa katika ofisi ya Nidhamu.**

II. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha , inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya Elimu Nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti Shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba ya Shule ni lazima
c) Kushiliki kwa Umakini kufanya maandalio ya jioni(preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za Shule na nyingine utakazopewa;
e) Kufahamu Mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika Shule hii;
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya Shule;
g) Kuvaa sare ya Shule wakati wote unapotakiwa;
h) Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote;

i) Kutunza mali za Umma.

III. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE:

a) Wizi
b) Uasherati na Ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya, kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga.
f) Kuharibu kwa makusudi mali za umma.
g) Kudharau Bendera ya Taifa.
h) Kusababisha mimba au kupata mimba.
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa Shule au watu
l) Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Kumiliki simu ya mkononi
n) Kumiliki simu au kutumia bila ruhusa maalumu
o) Kuharibu miundombinu au kusababisha uharibifu, mzazi atawajibika kulipa, kutengeneza au mwanafunzi kufukuzwa Shule

IV. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI:

a) Medical Examination form. Ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Selikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti Shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa mengine ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na Shule.

V. TAFADHARI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/ MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.

_____

VITUCE .J. MPOGOLE
MKUU WA SHULE

MEDICAL EXAMINATION FORM:

To be completed by a Medical Officer in respect of all form I or V entrants and new School employees

Full Name: ……
Age: …….. Year …….. Sex ……
Blood Cont (Red and White) ……
Stool Examination: ……
Analysis ……
Syphilis Test: …….
T. B. Test: ……..
Eye Test: ……
Ears: …….....
Abnomen: …….

ADDITIONAL INFORMATION: - e.g. Physical defect of impairment (s)
Infections, Chronic or family disease.

……
……
……
I certify the above is fit/ unfit to pursue his/ her lessons/ duties as required

Signature: ……
Designature: ……
Station: ……

Date: ……
NOTE: Medical Officer: At the time of Examination, Please treat the individual for any treatment ailments you note. Pupils/ Employee. This completed form should be sent to the school with your Acceptance Form of brought when you come to the School. No pupils and Errol, nor person any employed with certification or physical fitness

Delete as necessary.